**Nambari ya Mtahiniwa ______________________**

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**133** **KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2.00** **JUMAPILI 20 DISEMBA, 2020 MCHANA**

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. **Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
5. **Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| 12. | | |
| JUMLA | | |

**Mtihani huu una kurasa 13 zenye maandishi**

**Nambari ya Mtahiniwa ____________________**

## SEHEMU A: (Alama 15)

## UFAHAMU

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. **Soma habari hii kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kujifunza lugha ya Kiswahili hadi kujipatia utaalamu na ujuzi si mzaha. Ni harakati na mikakati ya kuuma meno hasa. Mwanafunzi anayeweza kujifunza Kiswahili mpaka afikie kilele cha mafanikio anahitajika kuwa makini sana. Awe msikivu, mdadisi na mtafiti wa kila suala linalohusu Kiswahili. Asiwe mwenye papara, mwenye kurukia maneno bila ya kuyachunguza ili ajue kama yanayozungumzwa ni maneno sanifu au lugha ya mitaani inayozungumzwa kiholela na wapita njia wa tua tugawe.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya kipekee. Msemaji mzuri wa Kiswahili sio yule anayenuia kupitisha ujumbe tu, bali ni yule anayepitisha ujumbe kwa namna inayofaa ili ueleweke kikamilifu. Hii hutegemea hasa na uteuzi mzuri wa msamiati.

Aidha, matamshi safi ni muhimu sana katika mawasiliano yoyote yale ya lugha ya Kiswahili. Matamshi yaliyojaa athari ya lugha mama hutatiza mawasiliano kutokana na kupotosha maana sahihi iliyokusudiwa na mzungumzaji lakini pia huleta maudhi na kumchosha msikilizaji. Tofauti na baadhi ya lugha nyengine, matumizi ya lugha sanifu katika Kiswahili huvutia sana kutokana na uzingatiaji wa ngeli pamoja na kuwa na msamiati mpana na unaoendelea kupanuka siku baada ya siku.

Lugha ya Kiswahili ina utajiri mkubwa wa methali, nahau, misemo, mafumbo na tamathali za semi. Msemaji hodari wa Kiswahili anafahamu matumizi murua ya semi na tamathali za semi. Matumizi hayo ni pamoja na uteuzi sahihi wa semi na tamathali hizo, wakati gani atumie kutegemea na mazingira, pamoja na ujumbe anaokusudia kuuwasilisha.

**Maswali**

a) Bainisha mambo mawili (2) yanayohitajika ili kupata utaalamu na ujuzi wa lugha ya Kiswahili.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b) Msemaji mzuri wa lugha ya Kiswahili ana sifa gani?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c) Matamshi yaliyojaa athari ya lugha mama yana athari gani katika mawasiliano?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

d) Eleza faida ya matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili katika mawasiliano.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

e) Ni yepi matumizi mazuri ya methali na misemo ya Kiswahili?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Fupisha habari uliyoisoma hapo juu kwa maneno yasiyozidi arubaini (40).

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU B: (Alama 40)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii. Swali la SITA (6) ni la lazima.**

3. a) Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo.

   i. T+H+N

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ii. N+V+T+E

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   iii. E+N+TS+TS+T+E

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   b) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya umoja.

   i. Vyumba hivi vya madarasa ni vidogo.

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ii. Hizi ndizo siku tulizokuwa tukizisubiri kwa hamu.

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

4. a) Tunga tungo yenye vipashio vifuatavyo kwa kutumia kiunganishi kilichomo ndani ya mabano. Nambari moja (i) imetumika kama mfano.

    i. Kirai na kirai (na)

    Katikati ya msitu **na** mlima mrefu.

    ii. Kitenzi na kitenzi (kisha)

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    iii. Sentensi na sentensi (pia)

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    iv. Nomino na nomino (au)

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ____________________________________________

b) Kwa kutumia mifano eleza maana ya istilahi zifuatazo.

    i. Vihusishi

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ii. Vihisishi

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ____________________________________________

    ____________________________________________

5. a) Andika neno lisilohusiana na mengine katika makundi yafuatayo.

i. Nyama, samaki, pweza, kome

______________________________________________

ii. Machungwa, mashelisheli, chenza, mabalungi

______________________________________________

iii. Tanzania, Kenya, Ujerumani, Kiingereza

______________________________________________

b) Taja sifa mbili (2) za ufupisho wa habari.

i. ______________________________________________

ii. ______________________________________________

6. a) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Elfu tisa mia tisa na tisa.

______________________________________________

ii. Laki nane, elfu sita na mia saba.

______________________________________________

iii. Milioni kumi na tatu, laki moja na mia moja.

______________________________________________

b) Tafsiri sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiingereza.

i. Mungu wangu! Nimesahau kuandika jina langu.

______________________________________________

______________________________________________

ii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina Wizara kumi na saba.

______________________________________________

______________________________________________

7. a) Eleza aina tatu (3) za washiriki wa mdahalo.

______________________________________________

______________________________________________

b) Taja dhima mbili (2) za mdahalo.

i. 

ii. 

**SEHEMU C: (Alama 30)**

**FASIHI**

**Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.**

8. Tunga beti tano (5) za ngonjera inayohusu jambo lolote lenye faida kwa jamii yako.

9. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za kifasihi.

i. Utenzi

ii. Fasihi

iii. Kibwagizo

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza maana ya methali zifuatazo.

i. Mvumilivu hula mbivu.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

ii. Kikulacho ki nguoni mwako.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

10. Eleza tofauti tano (5) kati ya mashairi na tamthiliya.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**SEHEMU D: (Alama 15)**

**UTUNGAJI**

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.**

11. Tunga Insha ya maneno kati ya 120 – 130 kuhusu "Athari za uvunjaji wa amani katika nchi yetu".

12. Andika mdahalo wenye hoja nne (4) ukitetea mada inayosema, "Matumizi ya simu za mkononi kwa wanafunzi yanaleta hasara zaidi kuliko faida".

==========================